



## KAMPUNI YA KIBO SEED

Marudio ya Tangazo la zabuni ya kuuza Magari na Pikipiki. Zab Na.  
KSCL.DOA/01/2024-2025.

Kampuni ya kibo seed imedhamiria kuuza Magari na Pikipiki yaliyokwisha kutumika. Waombaji wa zabuni wanashauriwa kukagua Magari na Pikipiki ambayo yanayouzwa katika hali yaliyonayo kwa sasa na sehemu yalipo bila dhamana ya muuzaji.

Mali zinazouzwa ni:

1. T933 DCQ FORD RANGER DOUBLE CABIN
2. T455 DKX FORD RANGER DOUBLE CABIN
3. T102 DCJ FORD RANGER PICKUP
4. T875 ANB NISSAN HARDBOARD DOUBLE CABIN
5. MC990 AMM YAMAHA
6. MC985 AMM YAMAHA

Waombaji wa zabuni wanaweza kuangalia na kukagua magari na pikipiki yanayouzwa katika ofisi za kampuni ya kibo seed siku za kazi Jumatatu hadi ijumaa kuanzia saa 02:00 Asubuhi mpaka saa 11:00 Jioni.

Zabuni zote ziwasilishwe kabla au tarehe **15/10/2024 saa 04:00 Asubuhi** bila kuchelewa zaidi ya hapo zikiwa ndani ya bahasha iliyofungwa na nje kuandikwa **ZABUNI YA KUUZA MAGARI NA PIKIPIKI. ZAB NA. KSCL/DOA/01/2024-2025** ndani ya box la zabuni linalopatikana mapokezi Kibo Seed Makao makuu Arusha, Mtaa wa Okaseni kuacha Barabara ya Arusha-Namanga.

Zabuni zilizowasilishwa zitafungulia tarehe **15/10/2024 saa 04:00 Asubuhi** katika chumba cha mikutano Kibo Seed na wahusika wanaruhusiwa kuhudhuria na kushuhudia.

### Vigezo vya kutathmini zabuni

Na.	Vigezo	Amekidhi/Hajakidhi vigezo (NDIO/HAPANA)
1.	Kujaza na kukamilisha jedwali kwa kuandika jina la mali inayonunuliwa na bei ya kununulia (iwe imesainiwa)	
2.	Zabuni yenye bei kubwa zaidi	

### SEHEMU YA 1. MASHARTI YA ZABUNI.

- 1.1 Mzabuni aliyefanikiwa kukidhi vigezo vyote atatakiwa kulipa 100% ya kiasi/bei

iliyoainishwa kwenye zabuni ndani ya masaa 72 baada ya kupokea barua inayomjulisha kwamba ameshinda

- 1.2** Mzabuni aliyeshinda atatakiwa kuchukua Magari/pikipiki alizolipia ndani ya siku kumi na nne (14).

**SEHEMU YA 2. TAARIFA ZA MZABUNI, MALI INAYONUNULIWA, NA BEI**

Taarifa hizi lazima zijazwe na ziwasilishwe. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kutokukidhi vigezo vyta zabuni.

Tarehe.....

Zabuni Na.....

Kwa: .....

**[Jina na anuani ya Kampuni iliyotangaza zabuni]**

Mimi/Sisi.....(Mtu binafsi/Jina la Kampuni).

1. Tumepitia/Nimepitia na kuelewa zabuni ya kuuza magari na pikipiki na  
Tumekubali/Nimekubali kununua pikipiki au magari kama inavyoonyesha hapa:

NA.	MAGARI/PIKIPIKI	BEI YA KUNUNULIA (TSH)
1.	T933 DCQ FORD RANGER DOUBLE CABIN	
2.	T455 DKX FORD RANGER DOUBLE CABIN	
3.	T102 DCJ FORD RANGER DOUBLE CABIN	
4.	T875 ANB NISSAN HARDBODY DOUBLE CABIN	
5.	MC990 AMM YAMAHA	
6.	MC985 AMM YAMAHA	
	<b>JUMLA</b>	

Jumla TZS..... [Jumla ya bei za  
kununua kiasi kwa maneno na tarakimu].

2. Tunakubali/Nakubali Kulipia kiasi tajwa hapo juu kama zabuni yangu itakubalika na kukidhi vigezo vilivyoainishwa.

Tarehe .....Siku ya ..... 20.....

Imesainiwa na.....  
(Mtu binafsi/Kampuni).